WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA)

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria No.2 ya mwaka 2018.

Kwa mujibu wa sheria ya hiyo, Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala ina mamlaka ya kuajiri wafanyakazi wa Wakala kwa mujibu wa kifungu Namba 5(g) cha Sheria ya Wakala Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

Hivyo, Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) inakaribisha maombi ya kujaza nafasi tupu katika Kada mbali mbali kwa waombaji wenye sifa stahili katika Ofisi yake iliyopo Maruhubi Unguja na Pujini Chake Chake Pemba.

Nafasi zenyewe ni kama zifuatazo;

UNGUJA

1. **MHANDISI MITAMBO DARAJA LA II (ZPSG-08) nafasi moja**

Sifa za muombaji

- Awe ni Mzanzibari.
- Awe na Shahada ya kwanza katika fani ya Uhandisi Mitambo (Bachelor of Engineering in Mechanical Engineering) au Mitambo na Elektroniki (Bachelor of Egineering in Mechatronic Engineering) au fani nyingine inayolingana nayo kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**.**

MAJUKUMU:

1. Kusaidia kuzifanyia matengenezo madogo madogo mashine na vifaa vyengine vitakavyoletwa karakana au kama atakavyoelekezwa pamoja na kutoa taarifa pale anaposhindwa kufanya hivyo
2. Kuhakikisha kuwa vifaa vyote vilivyomo karakana vinawekwa katika utaratibu mzuri pamoja na kuingizwa katika 'ledger'
3. Kukagua usalama wa mashine na kuhakikisha kuwa mashine zote zinafanyakazi;
4. Kuweka daftari la kutoa au kuazima vifaa vya karakana
5. Kuhakikisha usalama wa karakana, boksi la huduma ya kwanza (First Aid kit) pamoja na vifaa vya kuzimia moto kuwa vinafanyakazi
6. Kusimamia usafi wa karakana kabla na baada ya matumizi
7. Kutoa ushauri juu ya upatikanaji wa machine bora kwa wazalishaji wa viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati

2. MHANDISI MAABARA DARAJA LA II (ZPSG-08) nafasi moja

Sifa za muombaji

- Awe ni Mzanzibari.
- Awe mwenye Shahada ya kwanza katika fani ya Teknolojia na Sayansi ya Maabara (Bachelor of Technology in Laboratory Science) au fani nyengine inayolingana nayo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

MAJUKUMU:

1. Kusimamia utoaji wa mafunzo ya uzalishaji yatakayofanyika katika maabara
2. Kuhakikisha kuwa vifaa na vyombo vitakavyotumika kwa ajili ya mafunzo ya vitendo vimekamilika;
3. Kuhakikisha kuwa vifaa vya usalama (fire extinguisher na First Aid kit) vipo na vinafanyakazi;
4. Kusimamia na kutoa maelekezo ya matumizi ya vifaa vya maabara kwenye maeneo ya uzalishaji yaliyo chini ya SMIDA
5. Kuandaa vitini kwa ajili ya mafunzo ya vitendo;

6. Kufuatilia kwa wajasiriamali waliohitimu mafunzo na wakapata alama za ZBS na ZFDA au mamlaka nyenginezo na kuziwekea kumbukumbu;
7. Kuhakikisha usalama wa vifaa na watumiaji wa maabara

3. MHANDISI COMPUTER DARAJA LA II (ZPSG-08) nafasi moja

Sifa za muombaji

- Awe ni Mzanzibari.
- Awe mwenye Shahada ya kwanza katika fani ya Mhandisi Kompyuta (Bachelor of Engineering in Computer Engineering/Science) au fani nyengine inayolingana nayo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

MAJUKUMU

1. Kufanya ukaguzi wa kawaida na kuhakikisha vifaa na mifumo ya kompyuta inafanya kazi vizuri;
2. Kubuni mifumo ya kompyuta
3. Kubuni program za komputa
4. Kutoa ushauri wa sifa za kimitambo (Technical specifications) za vifaa na kompyuta wakati wa kufanya manunuzi;
5. Kutambua na kutatua matatizo ya mifumo na programu inapoibuka
6. Kuhakikisha programu na vifaa vimetengenezwa kufikia malengo ya Wakala
7. Kutengeneza mfumo wa kuzifanyia matengenezo na masawazisho programu za Wakala;
8. Kufuatilia mwenendo wa teknolojia mpya na kuitumia fursa zilizomo kwa maendeleo endelevu ya Wakala;

4. AFISA TEKNOLOJIA CHAKULA NA USINDIKAJI DARAJA LA II (FOOD SCIENTIST) (ZPSF-02) nafasi moja

Sifa za muombaji

- Awe ni Mzanzibari.
- Awe mwenye Shahada ya kwanza katika fani ya sayansi na teknolojia ya usindikaji wa chakula (BSc. Food science and technology) au fani nyengine inayolingana nayo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

MAJUKUMU:

1. Kufanya uchambuzi wa bidhaa za chakula zitakazozalishwa na wenye viwanda ili kutambua viwango vya virutubisho,vitamin, mafuta, sukari au protini vilivyomo ndani ya chakula na kutoatipoti;
2. Kuthibitisha uthabiti wa malighafi pamoja na kutathmini usalama, ubora, na thamani ya lishe ya bidhaa zilizozalishwa wakati wa mafunzo na katika eneo la uzalishaji linalosimamiwa na Wakala;
3. Kusaidia kubainisha njia za kubadilisha au kuondoa viungio hatari au visivyofaa vya kwenye vyakula kama vile bacteria;
4. Kuhakikisha kuwa vyakula vinavyosindikwa vinafikia viwango vilivyowekwa na Serikali;
5. Kuanzisha mbinu bora za kisasa za usindikaji wa chakula;
6. Kusaidia katika kubuni mbinu bora za uandaaji wa bidhaa za vyakula mahususi ili kuhifadhi vitamini, virutubisho pamoja na kuongeza siha ya mwili kwa mlaji;
7. Kuhakikisha viwango vya usafi, ubora, usalama na usimamizi wa taka vinafikiwa ndani ya maeneo ya usindikaji wa chakula.
8. Kusaidia katika utekelezaji wa kanuni za viwanda na serikali kwa kukagua maeneo ya usindikaji wa chakula. Na kutoa ushauri unaofaa.

5. FUNDI SANIFU MITAMBO DARAJA LA III (ZPSE-10) nafasi moja

Sifa za muombaji

- Awe ni Mzanzibari.
- Awe mwenye Stashahada ya Ufundi Sanifu NTA – III na kuendelea katika fani ya Mitambo (Diploma in Mechanical Engineering) au fani nyengine inayolingana nayo kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia Kompyuta

MAJUKUMU:

1. Kufanya matengenezo madogo madogo ya mashine na vifaa vyengine na kutoa taarifa pale anaposhindwa kufanya hivyo;
2. Kuvikagua na kuhakikisha usalama wa karakana pamoja na vifaa vya kuzimia moto kama vinafanyakazi;
3. Kupokea na Kutoa taarifa kwa matukio ya uharibifu au maharibiko ya vifaa vya karakana kwa sehemu husika;

4. Kusaidia kubadilisha vipuri vilivyoharibika katika mashine na mitambo kama atakavyoelekezwa;
5. Kushiriki katika kuchonga vipuri kama atakavyoelekezwa na mkuu wake;
6. Kushiriki kuchonga vipuri na kuchomelea kwa lengo la kuunda au kukarabati mashine mbali mbali chini ya usimamizi;

PEMBA

1. MHANDISI VIWANDA DARAJA LA II (ZPSG-08) nafasi moja

Sifa za muombaji

- Awe ni Mzanzibari.
- Awe na Shahada ya kwanza ya Uhandisi Viwanda (Bachelor of Science in Industrial Engineering) au fani inayolingana nayo kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali;

MAJUKUMU:

1. Kushiriki katika ukaguzi wa viwanda na kutoa ushauri juu ya uendeshaji wa shughuli za uzalishaji katika viwanda
2. Kushiriki katika kukusanya takwimu za uzalishaji katika viwanda;
3. Kutoa ushauri elekezi na huduma kwa wazalishaji
4. Kuweka daftari la kupokea, kutoa au matumizi ya vifaa vya uzalishaji
5. Kushiriki katika kuandaa miradi yanayohusiana na maendeleo ya viwanda
6. Kushiriki katika udhibiti wa mchakato wa ukuzaji wa bidhaa za viwandani
7. Kuandaa ripoti za Utekelezaji

2. FUNDI MCHUNDO MITAMBO DARAJA LA III (ZPSB-06) nafasi moja
Sifa za muombaji

- Awe ni Mzanzibari,
- Awe mwenye Cheti cha Ufundi (VTA) katika fani ya Mitambo au fani nyengine inayolingana kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

MAJUKUMU:

1. Kufanya matengenezo madogo madogo ya mashine na vifaa vyengine na kutoa taarifa pale anaposhindwa kufanya hivyo;
2. Kuvikagua na kuhakikisha usalama wa karakana pamoja na vifaa vya kuzimia moto kama vinafanyakazi;
3. Kupokea na Kutoa taarifa kwa matukio ya uharibifu au maharibiko ya vifaa vya karakana kwa sehemu husika;

4. Kusaidia kubadilisha vipuri vilivyoharibika katika mashine na mitambo kama atakavyoelekezwa;
5. Kushiriki katika kuchonga vipuri kama atakavyoelekezwa na mkuu wake;
6. Kushiriki kuchonga vipuri na kuchomelea kwa lengo la kuunda au kukarabati mashine mbali mbali chini ya usimamizi;

NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Muombaji anatakiwa aandike barua ya maombi kwa mkono na kuambatanisha na barua hiyo vitu vifuatavyo;

a) Vivuli vya vyeti vya kumalizia masomo.
b) Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa.
c) Maelezo binafsi ya Muombaji (CV)
d) Kivuli cha Kitambulisho cha Mzanzibari.
e) Picha moja ya Muombaji (Passport size).

MAMBO YA KUZINGATIWA

i. Muombaji atakaewasilisha “Statement of Result” au “Progressive Report” maombi yake hayatazingatiwa.
ii. Muombaji anatakiwa aainishe nafasi moja anayoiomba kati ya zilizotajwa hapo juu vinginevyo maombi yake hayatazingatiwa.
iii. Asiwe muajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
iv. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono na ziwasilishwe moja kwa moja Ofisi ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) iliyopo Eneo la Maruhubi barabara ya Bububu jengo nambari 134 Unguja wakati wa saa za kazi.
v. Na kwa upande wa Pemba muombaji anatakiwa awasilishe ombi lake moja kwa moja Ofisi ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) iliyopo Pujini Chake Chake Pemba wakati wa saa za kazi.
vi. Siku ya mwisho ya kupokea maombi ni Ijumaa tarehe 29 Disemba, 2022 saa 9.30 alaasiri.
vii. Mawasiliano yatafanywa kwa wale tu watakaopita katika mchujo wa awali (short listed).
viii. Aidha muombaji mwenye sifa za ziada atazingatiwa zaidi.

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MKUU,
WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO,
VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA),
S.L.P 1966,
MARUHUBI BARABARA YA BUBUBU
JENGO NAMBARI 134
MKOA WA MJINI MAGHARIBI
ZANZIBAR.

NAMBARI YA SIMU +255 242 232 880

Tangazo hili linapatikana pia katika
Tovuti ya Wakala: www.smida.go.tz.
Tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini:

Pamoja na mitandao ya kijamii ya Wakala ifuatayo:
Facebook: @facebook.com/smidaviwanda
Instagram: @smida_viwanda_zanzibar
Twitter: @SMIDAViwanda